JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKINOLOGIA

Simu: **+255** -0**766-888822**
/0754-366331 / 0260-2606261
E-mail: nyamweziteachers@yahoo.com
web: www.nyamweziteachers.ac.tz

Chuo Cha Ualimu Nyamwezi
S.L.P.1764
TABORA

USAJILI WA WIZARA YA ELIMU: CU. 148
USAJILI WA NACTE: REG/TLF/090

KUMB. NA. **NTC/JI/20/**0209

NDUGU:.....
S.L.P:.....

YAH: KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU ELIMU YA SEKONDARI(DIPLOMA) ,UALIMU ELIMU YA MSINGI NA UALIMU KAZINI/TARAJALI KWA MUHULA WA MASOMO 2020/2021

1.0 UTANGULIZI

Ninayofuraha kukujulisha kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknologia na ufundi chini ya Bodi ya NACTE imekuchagua kujiunga Stashahada ya Elimu ya Sekondari , stashahada ya Elimu ya Msingi na Stashahada ya Ualimu Kazini katika **Chuo cha Ualimu Nyamwezi kilichopoTabora mjini**.

Chuo kinakupongeza kwa nafasi hii na tunategemea kuwa utaitumia vizuri na kusoma kwa juhudi zako zote ili uweze kufanya vizuri katika mafunzo yako, kwa manufaa yako na ya Taifa kwa ujumla.

2.0 DIRA YA CHUO

MWALIMU MAHIRI ALIYE SHEHENI UJUZI, STADI ZA MAISHA NA KAZI.

3.0 DHAMIRA YA CHUO

“Kutoa walimu mahiri wenye maarifa, ujuzi na stadi wanaoweza kukabiliana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia na changamoto mbalimbali za maisha kisiasa, kijamii na kiuchumi.

3.1 Moto wa Chuo ni " **ELIMU UJUZI**

4.0 MAHALI CHUO KILIPO:

Chuo kipo **Tuli** Tabora mjini jirani na Kanisa la Romani Katoliki Ipuli ndani ya eneo la chuo cha Musoma Utalii - Tabora.

5.0 KUFUNGUA CHUO:

Unatakiwa kufika chuoni tarehe **26/ 10 / 2020** ili kuanza mafunzo kulingana na maelekezo ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknologia na ufundi**.**

6.0 MAFUNZO:

Masomo yanayofundishwa hapa chuoni ni masomo yote ya Ualimu, pamoja na masomo YOTE yanayofundishwa katika shule za Awali ,Msingi na Sekondari

8.0 MITIHANI

Kutakuwepo na majaribio ,mitihani ya mihula (Semester exams.) kila tunapokaribia kufunga chuo.Taarifa ya matokeo ya mitihani yako itawekwa kwenye mtandao ili uweze kuona popote ulipo.

Wanachuo wote watafanya mtihani wa Taifa (NECTA) mwishoni mwa kozi.

9.0 USAJILI:

Ufikapo chuoni unatakiwa kuripoti Ofisi ya Usajili uoneshe:-

Vyeti halisi (**Original)** vya kidato cha nne/Sita/ualimu Grade "A" (Results slip kwa wale ambao vyeti havijatoka) pamoja na vivuli vya vyeti hivyo (Photocopies)kwa matumizi ya ofisi.

Picha (Passport size)- 4,pamoja na File 1

- Kila mwanachuo anastahili kulipia sh 24,000/= kwa ajili ya karatasi (rim2)

Fomu ya kupimwa na daktari wa serikali (Medical Examination Certificate).

ADA YA CHUO

MCHANGANUO WA ADA NA MICHANGO YOTE MUHIMU YA CHUO

ADA NA MICHANGO MINGINE			
		MUHULA I	MUHULA II
	ADA +BWENI	**460,000/=**	**460,000/=**
Malipo ya Usajili		**30,000/=**	**-**
Tahadhari		**50,000/=**	**-**
Kitambulisho		**10,000/=**	**-**
T-shirt		**10,000/=**	**-**
Michezo		**30,000/=**	**-**
Ada ya Mitihani ya ndani kwa mwaka		**100,000/=**	**-**
Ada ya Mtihani wa NECTA		**50,000/=**	**-**
Uendeshaji Serikali ya Wanachuo		**10,000/=**	**-**
Utahini wa mafunzo kwa vitendo		**60,000/=**	**-**
	JUMLA	**810,000/=**	**460,000/=**

MUHIMU:

Malipo yote yaliyoorodheshwa katika fom yanatakiwa kulipwa kupitia **benki Account Number;**

CRDB: 0150260551000 JINA: NYAMWEZI TEACHERS COLLEGE.

11.0 MAZOEZI YA KUFUNDISHA

Kutakuwa na mazoezi ya kufundisha kwa vikundi (**Micro- teaching practice)** yatakayo kuwa yakifanyika chuoni na Maonyesho ya ufundishaji (Demonstration Lesson) na mazoezi ya ufundishaji wa muda mfupi **(Single lesson teaching Practice)**

Pia kutakuwa na mafunzo ya muda mrefu kwenye shule mbalimbali nje ya eneo la chuo (**BTP**)

12.0 MALAZI: Kwa wale wa bweni

Unatakiwa kuja na:-

- Godoro 3X6
- Shuka mbili (2) za rangi ya Pink au Blue bahari,
- Mto na foronya moja ya rangi ya Pink au Blue Bahari
- Chandarua na ndoo ya kuogea.

13.0 VIFAA VYA TAALUMA.

Unatakiwa kuleta vifaa vyote muhimu kwaajili ya Taaluma ikiwa ni pamoja na:- **Daftari zisizopungua 06 .**

14.0 MALI BINAFSI. Kila mwanachuo anatakiwa kutunza mali zake binafsi.

SARE YA CHUO

Suti nyeusi, sharti jeupe la mikono mirefu na viatu veusi

MAVAZI YA KUSHINDIYA

- Traki suti rangi ya blue bahari
- Raba za michezo

NB. Ni lazima mwanachuo aje amevaa Traki rangi ya Blue bahari suit na raba za michezo

15.0 SHERIA NA TARATIBU ZA CHUO.

- **.** Makosa yanayoweza kusababisha mwanachuo kuachishwa masomo (kufukuzwa).
- **.** Wizi,Uasherati,Ulevi au utumiaji wa aina yoyote ya madawa ya kulevya.
- **.** Kuharibu kwa makusudi mali ya chuo
- **.** Makosa ya jinai
- **.** Kupigana
- **.** Kufeli masomo
- **.** Kugoma, kushiriki au kushawishi mgomo

16.0 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANACHUO KURUDISHWA NYUMBANI

- **.** Kutohudhuria vipindi kwa asilimia thelathini (30%) ya muhula au kutoingia darasani siku saba (7)mfululizo bila sababu ya msingi au kutohudhuria "Prep" kwa wale wa bweni.
- **.** Kutofikisha alama 50% kwa somo baada ya kurudia au kukataa kurudia masomo aliyoshindwakufikisha 50%

Kulala nje ya Hostel

Kuwa katika mahusiano ya kimapenzi

Tunakutakia maandalizi mema ya kujiunga nasi na tunakukaribisha sana chuo cha ualimu Nyamwezi – Tabora.

.....

ROBERT MAGERE

MKUU WA CHUO